



# Haki zako katika Victoria na mtu anayeweza kukusaidia

## Haki za Binadamu

Katika Victoria ni kinyume cha sheria kwa mtu yeyote kukubagua kwa sababu ya rangi yako, dini, jinsia, imani ya kisiasa na mambo mengine mengi. Una haki zingine pia kama vile haki ya kuwa salama, kudhaminiwa, kuabudu dini yako na kufurahia utamaduni wako na familia.

Hizi huitwa 'haki za binadamu' na kila mtu ana haki sawa katika Victoria, bila kujali popote alipozaliwa.

## Ubaguzi

Pia ni kinyume cha sheria kwa wewe kudhaminiwa tofauti au isivyostahili kama ikitokea katika maeneo kama ya kazi yako, wakati wa kukodisha nyumba, shuleni, dukani, mgahawani au wakati wa kucheza mchezo.

Watu hawawezi kukuthamini isivyostahili eti kwa sababu:

- ya rangi ya ngozi yako, tamaduni au rangi, historia ya familia yako au nchi unayotokea
- ya dini yako, imani ya dini au shughuli. Kwa mfano, watu hawawezi kukuchukulia tofauti kwa sababu ya kwenda msikitini, kwenye sinagogi au kanisani. Unaruhusiwa kutokuwa na dini yoyote
- ya kuwa na ulemavu, ugonjwa au kuumia. Kwa mfano, kama una ulemavu au ugonjwa unaweza kuomba mipangilio mbalimbali ya kazi bila ya kuadhibiwa na boshi wako anahitaji kufanya mipango ya kuridhisha hivyo ili uweze kufanya kazi yako
- kama wewe ni mzazi au mlezi. Kwa mfano, kama unalea watoto au ndugu wa familia unaweza kuomba kufanya kazi kwa masaa tofauti au kuwa na muda wa kupumzika ili kuwatunza watoto au familia

- ya umri wako. Kwa mfano, kama ukiomba kazi hawawezi kusema wewe ni mzee sana au mdogo sana kwa ajili ya kazi
- wewe ni mwanaume au mwanamke
- una mimba au kunyonyesha. Kwa mfano, una haki ya kumnyonyesha mtoto katika nafasi ya umma kama vile mgahawani au uwanja wa michezo, unaweza kuchagua kufanya kazi wakati ukiwa mjamzito au ukiwa bado unanyonyesha
- ya shughuli za kujamiiana ambazo zinakubalika kisheria. Kwa mfano, huwezi kuchukuliwa isivyo haki kwa sababu ya mtu ambaye unafanya mapenzi naye
- ya upendeleo wako wa kimapenzi au utambulisho wa kijinsia. Kwa mfano, mashoga, wasagaji, jinsia mbili, jinsia tofauti, kubadili jinsia na watu wa jinsia mbalimbali wote wana haki
- ya kuolewa au kutoolewa. Haijalishi kama una ndoa, umetoa talaka, hujaolewa au kuishi pamoja, ni lazima utendewa haki
- ya maumbile ya kimwili. Kwa mfano, huwezi kudhaminiwa kwa sababu ya urefu, uzito, kiasi, nywele au alama za kuzaliwa
- ya matendo yako kuhusu haki katika kazi. Kwa mfano, huwezi kufukuzwa au kuadhibiwa kwa kuuliza maswali au kuzungumza matatizo uliyonayo kazini

- shughuli za vyama vya wafanyakazi. Kwa mfano, huwezi kufukuzwa kazi kwa sababu ni mwanachama wa chama cha wafanyakazi au kwenda kwenye mgomo
- siasa yako, imani ya kisiasa au shughuli au kwa sababu hujishughulishi katika shughuli za kisiasa

Pia ni kinyume cha sheria kwa wewe kudhamini mtu mwingine tofauti kwa sababu yoyote kati ya hizi.

Kama ungependa habari zaidi juu ya haki zako za binadamu au juu ya ubaguzi na nini unaweza kufanya kama unahitaji msaada, unaweza kupigia Tume kwa **1300 292 153** au kwa mkalimani, tafadhali piga simu **1300 152 494**.

Huwezi kuadhibiwa au kutokutendewa haki kwa kutuuliza msaada au kufanya malalamiko, na ni watu tu waliohusika katika malalamiko watajua kuhusu hilo. Kuwakilisha malalamiko haina maana kuwa utakwenda mahakamani.

Unaweza pia kutembelea

**humanrightscommission.vic.gov.au** kwa habari zaidi. Tunatoa pia habari za bure juu ya haki zako katika maeneo ya umma, kazini na katika mashirika ya serikali.



**Victorian Equal Opportunity  
& Human Rights Commission**

### Need more information?

Contact the Commission:

Enquiry Line 1300 292 153 or (03) 9032 3583  
 Fax 1300 891 858  
 TTY 1300 289 621  
 Email [enquiries@veohrc.vic.gov.au](mailto:enquiries@veohrc.vic.gov.au)  
 Website [humanrightscommission.vic.gov.au](http://humanrightscommission.vic.gov.au)

### Accessible formats

This publication is available to download from our website at [humanrightscommission.vic.gov.au/resources](http://humanrightscommission.vic.gov.au/resources) in PDF and RTF. Please contact the Commission if you require other accessible formats.

### We welcome your feedback!

Were these resources useful? Easy to use? Would you like to see something else included? Please email us at [communications@veohrc.vic.gov.au](mailto:communications@veohrc.vic.gov.au).

Published by the Victorian Equal Opportunity and Human Rights Commission, Level 3, 204 Lygon Street, Carlton Victoria 3053. May 2013.

Disclaimer: This information is intended as a guide only. It is not a substitute for legal advice.